# WATU NA WAKUSHUKURU

Zab. 66 : 1-2, 4-5, 7 (K) 5

**Wimbo wa Katikati**
**Jumapili ya 20, Mwaka A**

Rogers K. J
August, 2023
Dodoma




1. Mungu na atufadhili na kutubariki, na kutuangazia uso wake/
   Njia yake ijulikane duniani, wokovu wake katikati ya mataifa yote.

2. Mataifa na washangilie, Naam, waimbe kwa furaha/
   Maana kwa haki utawahukumu watu, na kuwaongoza mataifa walioko duniani.

3. Watu na wakushukuru Ee Mungu, watu wote na wakushukuru/
   Mungu atatubariki sisi, miisho yote ya dunia itamcha Yeye.